

ISHARA YA UMOJA `22

Fr. Kashakuro.



1. Kri stu a li tu pe nda kwe li a ka tu pe nda u pe o,



a ka tu we ke a E ka ri sti, Mwi li na Da mu ya ke.

I sha ra ya u mo ja pi a ki fu ngo cha ma

pe - - - ndo Hi i E ka ri - - - sti.

2. Katika karamu ya mwisho Yeye na mitume wake/ ndipo alipoweka hii sakramenti takatifu
3. Alitwaa mkate akaubariki akawapa/ Akasema twaeni mle huu ndio mwili wangu.
4. Akakitwaa kikombe akashukuru akawapa/ akasema- nyweni nyote hii ndiyo damu yangu.
5. Kisha aliwaamuru kuadhimisha Ekaristi/ "Fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu".
6. Alituamuru kupendana ili kumshuhudia/ Pendaneni watawatambua mu wafuasi wangu
7. Basi kikombe kile cha baraka chatuunganisha/ Ili tuwe umoja kama Baba, Mwana naye Roho.
8. Amani, furaha, upendo, uvumilivu msamaha/ na umoja tuvikute katika Ekaristi hii.